Matumizi ya mifuko ya plastiki inavyoathiri mazingira na afya

Mwaka 2013 serikali ilipiga marufuku matumizi yote ya mifuko ya plastiki isipokuwa ile yenye unene wa maikroni 100 na vifungashio vya bidhaa mbalimbali kama vile vya hospitalini.

Awali Serikali iliruhusu matumizi ya mifuko yenye unene wa maikroni 30 lakini kutokana na wananchi kutokuwa na uwezo wa kupambanua na ile iliyopigwa marufuku wafanyabiashara wengi walitumia mwanya huo kuichanganya.

Serikali kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) mwaka 2013 ilitoa muda wa miezi mitano tangu sheria ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki.Hata hivyo hadi sasa bado matumizi ya mifuko hiyo hatari yanaendelea katika nchi nzima.

Yamefanyika marekebisho ya kanuni iliyokuwa inaruhusu matumizi ya mifuko yenye ujazo wa maikroni 30 ambapo adhabu zake zitakuwa kubwa kwa yeyote atakayekutwa na mfuko uliopigwa marufuku.

Ili kuhakikisha kwamba uchafuzi wa mazingira kutokana na mifuko ya plastiki unadhibitiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa kushirikiana na wadau, imeandaa Rasimu ya kanuni mpya ya mifuko ya plastiki inayoongeza unene wa mifuko kutoka maikroni **30** na kufikia maikroni **50**.

Mifuko yenye unene chini ya mikroni **50** haitaruhusiwa kuzalishwa, kuingizwa nchini wala kutumika. Chini ya Kanuni hii baadhi ya bidhaa za

plastiki (Polyethelyne materials) itaendelea kutumika kwa ajili ya shughuli muhimu viwandani, kama vile viwanda vya maziwa, na usindikaji wa vyakula.

Uchunguzi umebaini kuwa mifuko ya plastiki ni hatari katika mazingira kwa sababu haiozi na inaweza kuleta madhara makubwa katika mazingira na afya.

Madhara ya mifuko ya plastiki

Wataalam wa mazingira wanayataja madhara yanayosababishwa na matumizi ya mifuko ya plastiki kuwa ni kuua udongo,kuzalisha gesi za sumu,kuleta matatizo kwenye mifumo ya uzazi,mifumo ya hewa, magonjwa ya figo,saratani,na magonjwa mengine mengi.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mfumo wa Upumuaji Dk Meshack Shimwela anasema moshi unaosababishwa na uchomaji wa mifuko ya plastiki huleta magonjwa yanayoongoza kwa kuua watu wengi katika nchi maskini duniani.

Tafiti mbalimbali za kisayansi zinaonesha kuwa, uchomaji wa plastiki kwa sababu yoyote ile, husababisha madhara kwa afya ya jamii na mazingira kwa sababu ya kuzalisha moshi wenye sumu mbalimbali zinazochafua hewa.

Kwa kutambua hatari za kiafya zinazotokana na sumu za moshi wa mabaki ya plastiki, Shirika la Afya Duniani (WHO) liliadhimia makubaliano ya Stockholm Sweden ya mwaka 2001 ya kupunguza uzalishaji wa moshi wenye sumu,yanatekelezwa katika nchi zote wanachama wa Umoja wa Mataifa.

Serikali inatambua uwepo wa madhara yatokanayo na matumizi ya mifuko ya plastiki ndiyo maana imewekwa kanuni na sheria za kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na mifuko ya plastiki.

Jambo la kusitikisha ukizunguka katika maeneo mbalimbali mijini na vijijini utakuta mifuko ya plastiki maarufu kwa jina la Rambo ikizagaa kila mahali huku mingine ikichomwa moto na moshi wake ambao unasababisha maangamizi makubwa ukizagaa angani.

Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ni wadau muhimu nchini ambao wanaendesha mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira na kuhakikisha kuwa mazingira yanatunzwa.

NEMC wanataja sababu ya kuzagaa kwa mifuko ya plastiki hapa nchini kuwa ni kutokana na kutupwa hovyo mara baada ya kutumika.

Hata hivyo kwa mujibu wa taarifa ya NEMC sio mifuko yote ya plastiki ambayo imepigwa marufuku na serikali katika sheria hiyo ya mazingira nchini ndiyo maana baadhi ya mifuko inaendelea kuingizwa nchini na kuuzwa.Hata hivyo serikali imepiga marufuku matumizi ya mifuko yote ya plastiki kutokana na athari kubwa za kimazingira zinazosababishwa na mifuko hiyo.

Kenya yapiga marufuku mifuko

Serikali ya Kenya imeanza kutekeleza marufuku ya mifuko ya plastiki nchini humo baada ya juhudi za miaka mingi za kutaka kuipiga marufuku bila mafanikio. Serikali ya Kenya ilikuwa imetoa muda wa miezi sita kwa wadau kujiandaa kabla ya kuanza kutekelezwa kwa marufuku hiyo.

Juhudi za watengenezaji wa bidhaa za mifuko ya plastiki kuomba muda zaidi kabla ya kutekelezwa kwa marufuku hiyo kortini ziligonga mwamba baada ya ombi la kucheleweshe marufuku hiyo kukataliwa na mahakama kuu.

Kenya imeamua mtu yeyote anayepatikana akitengeneza, kuuza au kutumia mifuko hiyo ya plastiki anaweza kupigwa faini ya hadi dola 40,000 au kufungwa jela hadi miaka minne.

Serikali ya Kenya imesema marufuku hiyo itasaidia kulinda mazingira.Lakini watengenezaji wa bidhaa wamesema marufuku hiyo itasababisha kupotea kwa nafasi 80,000 za kazi.

Wakenya hutumia takriban mifuko 24 milioni ya plastiki kila mwezi, kwa mujibu wa takwimu za serikali.

Nchi nyingine katika Bara la Afrika ambazo zimepiga marufuku mifuko ya plastiki ni Afrika Kusini, Rwanda na Eritrea.

Hili ni jaribio la tatu la kupiga marufuku mifuko hiyo nchini Kenya katika kipindi cha miaka kumi.Serikali ya Kenya imekuwa ikihimiza wateja kuanza kutumia mifuko mbadala ambayo haijaundwa kwa kutumia plastiki.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Taifa ya Mazingira ya Kenya, wasafiri wanaopakia bidhaa walizonunua katika maduka yasiyotozwa kodi watalazimika kuiacha mifuko hiyo ya plastiki uwanja wa ndege kabla ya kuruhusiwa kuingia.

Mifuko inayofaa kwa matumizi

NEMC inawashauri wananchi wa Tanzania, kutafuta aina nyingine ya mifuko ambayo haina athari za kimazingira na hivyo kuachana na mifuko ya plastiki ambayo imeonekana dhahiri kuleta madhara kiafya na kimazingira.

Mifuko inayoshauriwa kutumika kwa mujibu wa wataalam wa mazingira ni mifuko ya karatasi,vikapu na mifuko ya nguo ambayo haina madhara kabisa katika mazingira.

Kutokana na madhara makubwa ya mifuko ya plastiki ni vema wafanyabiashara na wenye maduka kuacha biashara ya mifuko ya plastiki badala yake waanze kuuza mifuko ya karatasi na vikapu vya asili.

NEMC inashirikiana na wadau wa mazingira zikiwemo taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali ili kuweza kusaidia kutengeneza kwa wingi mifuko ya asili na hivyo kutunza mazingira.

Utafiti umebaini kuwa mifuko ya asili na ambayo sio ya plastiki matumizi yake ni endelevu na inaweza kutumika mara nyingi na kufanyiwa urejereshaji(Recycling) jambo ambalo haliwezekani katika mifuko ya plastiki.

Historia inaonesha kuwa tangu kuingia kwa mifuko ya plastiki nchini, watu wengi wameacha utamaduni wa kutumia mifuko ya karatasi na nguo iliyotengenezwa kwa rasilimali za asili.

“Ni vema sasa wananchi wangerudisha utamaduni wa kuanza kutumia tena vifaa vya asili na kuachana na mifuko ya plastiki ambayo ina madhara kimazingira na kiafya’’, anasisitiza Mwanamazingira Vikta Komba kutoka Wilaya ya Nyasa.

Ametoa wito wa kuhakikisha kuwa mifuko ya plastiki isiyokuwa na viwango haitumiki tena na kuwachukulia hatua watakaokamatwa na mifuko ya plastiki kuwa ni kosa la jinai kulingana na sheria .

Komba anasisitiza kuwa Mkoa wa Ruvuma una bahati ya kuwa na rasilimali nyingi za asili ambazo zinaweza kutumika kutengenezea vikapu, mikeka, vijomela, majamanda, ungo,madengu na matenga hivyo kuacha kutumia mifuko ya plastiki ambayo ni adui wa mazingira.

Kwa kuwa wataalam wa kutengeneza vifaa hivyo vya asili wapo katika jamii ameshauri ni vema ufundi huo wa kusuka vifaa vya asili kama vile vikapu na bidhaa nyingine za asili kuwarithisha watoto na vijana ili viwe endelevu.